

**HOTUBA YA MKUU WA CHUO KATIKA MAHAFALI YA 41 YA CHUO CHA  
ARDHI MOROGORO**

**TAREHE 14/04/2023**

Mhe. Geofrey Mizengo Pinda (Mbunge), Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi;

Mhe. Fatuma Mwassa, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro;

Mhe. Profesa Ernest Kihanga, Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo Cha Ardhi Morogoro;

Bw. Seushi Mburi, Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo cha Ardhi Morogoro;

Wajumbe wa Bodi ya Chuo cha Ardhi Morogoro;

Wakuu na Watendaji wote wa Taasisi na Idara za Serikali mliopo hapa;

Wajumbe wa Menejimenti ya Chuo cha Ardhi Morogoro;

Ndugu Wanahabari kutoka Vyombo Mbalimbali Vya Habari;

Wageni Waalikwa Wote, Mabibi na Mabwana.

**Habari za asubuhi!**

## **Ndugu Mgeni Rasmi,**

Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kuweza kufanikisha maandalizi ya sherehe ya mahafali ya 41 ya Chuo chetu. Kipekee ninakushukuru wewe Mgeni Rasmi, kwa kukubali mwaliko wetu na kujumuika nasi katika mahafali haya. Aidha, naomba nitumie fursa hii kutoa shukrani nyingi kwa viongozi na wageni wote mlajumuika nasi katika kusherehekeea mafanikio ya wahitimu wetu **329** wa fani za Jiomatikia na Mipango Miji, ambapo kilele cha furaha yao kinahitimishwa leo katika mahafali ya 41 ya Chuo cha Ardhi Morogoro.

Nasema, karibuni sana Chuo cha Ardhi Morogoro.

## **Ndugu Mgeni Rasmi,**

Sherehe za mahafali ya 41 ya Chuo cha Ardhi Morogoro hazikuweza kufanyika katika muda wa kalenda yetu (yaani tarehe 24 Novemba 2022) kutokana na sababu zilizokuwa nje ya uwezo wetu. Tunaushukuru Uongozi wa Wizara yetu kwa kushughulikia changamoto iliyokuwepo na hatimaye leo tumefanikiwa kujumuika pamoja kwa ajili ya mahafali ya wahitimu wetu.

## **Ndugu Mgeni Rasmi,**

Naomba kutaja mafanikio machache ambayo Chuo chetu kimeyapata tangu kuanzishwa kwake:

### **1) Ongezeko la udahili**

Wanafunzi waliodahiliwa tangu Chuo kianzishwe mwaka 1978 ni **5109** wa jinsia ya kike ni **1009 (20%)** na wa kiume ni **4100 (80%)**. Kati ya hao, wanafunzi **4334 (87%)** waliweza kumaliza masomo kwa mafanikio ambapo wa jinsia ya kike ni **743 (15%)** na jinsia ya kiume ni **3591 (72%)**.

## **Ndugu Mgeni Rasmi,**

Wakati kinaanzishwa Chuo chetu kilikuwa na uwezo wa kudahili wanafunzi wasiozidi **60**, lakini kwa sasa kinao uwezo wa kudahili wanafunzi **660**; hivyo katika kipindi cha miaka **41**, uwezo wetu wa kudahili umeongezeka mara **11**.

Aidha, katika mwaka wa masomo 2022/2023 wanafunzi **349** wamedahiliwa kwa kozi ya Jiomatikia, ambapo wanafunzi wa kike ni **100 (29%)** na wa kiume wakiwa **249 (71%)**. Kadhalika, katika kipindi hiki wanafunzi waliodahiliwa kwa kozi ya Mipango Miji ni **147** ambapo wa kike ni **64 (44%)** na wa kiume ni **83 (56%)**.

## **2) Ongezeko la wahitimu**

Katika kipindi cha miaka 46 tangu Chuo kianzishwe, kimefanikiwa kuzalisha wahitimu wanaofikia **4,334**.

## **3) Ongezeko la mitaala**

Kwa kipindi cha miaka 41, yaani 1978 hadi 2018, Chuo cha Ardhi Morogoro kiliweza kuzalisha mafundi sanifu wa fani moja ya Jiomatikia (hapo wali ilijulikana kama Upimaji Ardhi). Katika miaka mitano (5) iliyopita, Chuo kimefanikiwa kuongeza kozi ya Mipango Miji, na kipo katika hatua za uandaaji wa mitaala ya Mifumo ya Taarifa za Kijiografia (*Geographic Information Systems*) pamoja na Usanifu Majengo (*Architecture*) ili kuendana na mahitaji ya soko.

**Ndugu mgeni Rasmi,**

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana tangu kuanzishwa kwake, Chuo cha Ardhi Morogoro kinazo changamoto kadhaa:

- a) **Uhaba wa wafanyakazi:** kwa muda mrefu, Chuo cha Ardhi Morogoro kimekuwa na uhaba wa wafanyakazi, hasa wakufunzi. Uhaba huu umekuwa ukishughulikiwa kwa kuajiri watumishi wa muda mfupi (part-time tutors).

- b) **Uhaba wa vifaa vyatukufunzia:** pamoja na ongezeko la udahili tuliloshudia kwa miaka ya hivi karibuni; tumekuwa na changamoto ya uhaba wa vitabu, kompyuta na vifaa vyatukufunzia (*GNSS receivers, total stations, levels*)..
- c) **Uhaba/ uchakavu wa miundombinu:** Chuo kimekuwa na changamoto ya uhaba wa vyumba vyatukufunzia madarasa, studio na ofisi za wafanyakazi. Hata hivyo, tunaendelea na ujenzi wa madarasa matatu katika kiwanja hiki tulipo hivi sasa, yenye uwezo wa wanafunzi 210 kila moja. Ujenzi wa madarasa ukikamilika, kituo hiki kitakuwa na uwezo wa kupokea wanafunzi 1290. Changamoto ya miundombinu itafikia tamati iwapo tutafanikiwa kutekeleza Mpango Kabambe (2023 – 2043) ambao umelenga kufanya maboresho ya miundombinu iliyopo katika kiwanja hiki na kuendeleza eneo letu lililopo Mlima Kola. Tukifanikiwa kutekeleza mpango huo, Chuo chetu kitakuwa na vituo viwili, yaani Kampasi ya Boma (*hapa tulipo*) na Kampasi ya Mlima Kola.

### **Ndugu Mgeni Rasmi,**

Naomba nihitimishe kwa kukuomba wewe na Wizara yako muendelee kukisaidia Chuo chetu katika utatuzi wa changamoto zilizobainishwa.

Mwisho, nakuomba Mwenyekiti wa Bodi nikukaribishe ili uchukue fursa hii kutoa hotuba yako na hatimaye umkaribishe Mgeni Rasmi aongee na hadhira hii.

### **Mheshimiwa Mgeni rasmi naomba kuwasilisha.**